

Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA KAZI YA
KIMISHENI ULMWENGUNI KOTE

MWANAMKE ALIYEVIKWA JUA

“Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili” (Ufunuo 12:1).

Mtume Yohana alipata heshima kubwa ya kupata maono ya utukufu wa mwanamke huyu huko mbinguni akiwa na mwangaza mkubwa uliong'ara sana. Maono haya yanapatikana katika kitabu cha Ufunuo na ni mfano ambao ndani mwake kuna ukweli muhimu. Wakati mwingi mwanamke huwa ni mfano unaowakilisha kanisa—kanisa la kweli au lisilo la kweli. Katika maono haya mwanamke huyu anaonyeshwa kama mtu aliye safi, kwa maana yeye alivikwa jua. Yeye anawakilisha usafi na utukufu wa kanisa la mitume. Mfano wake ni kinyume na mfano wa kanisa lililoanguka ambalo mfano wake unaonekana kwenye maono ya baadaye kupitia kwa mwanamke kahaba ambaye si mwaminifu kwa bwana wake.

Kwenye maono haya mwanamke huyu amesimama juu ya mwezi. Mwezi hauna mwangaza wake binafsi bali huangaza asilimia kidogo ya mwangaza wa kweli

ambao hutolewa na jua. Mwezi ni mfano unaofaa wa Agano la Kale ambalo lilikuwa “kivuli cha mema yatakayokuwa” (Waebrania 10:1). Agano hilo lilikuwa kiongozi na mwalimu wa kutuleta kwa Kristo



Kanisa la Mungu Lenye Utukufu

(Wagalatia 3:24-26). Agano lenyewe linatazamia jambo bora ambalo lingejiri baadaye.

“Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo” (Yohana 1:17).

Mwanamke huyu alivikwa utukufu wa jua. Jua huwa chimbuko la mwangaza wa kawaida katika mpangilie wa ulimwengu wetu. Wakati Kristo alikuja kwenye ulimwengu huu uliopotea jua lenye urembo mwingi wa ukweli lilichipuka ambalo lilifukuza giza lililokuwepo. Kristo ndiye chanzo cha mwangaza wa kiroho katika kipindi cha Agano Jipya. Mwangaza wa ukweli huangazia dhambi na kuonyesha njia ya kupata haki na ushindi. Kanisa la kweli limevikwa mwangaza mkubwa wa usafi na unashinda kwa mbali mwangaza hafifu wa kanisa la Agano la Kale.

Mwanamke huyu alikuwa na taji la nyota kumi na mbili. Taji hili linawakilisha mamlaka na nguvu za utawala. Kanisa la Mungu haliiongozwi au kufungwa na dhambi na badala yake linatawala kwa ushindi juu ya nguvu za adui, hata katika nyakati hizi zetu zenye uovu mwingi.

Hapo mbeleni mtume Yohana alikuwa
(Inaendelea kutoka ukurasa 2)

Tahariri

3

Kujifunza Biblia:
Kanisa la Mungu

4

Kanisa la Mungu

5

Maswali na Majibu

7

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

8

MAMBO AMBAYO

BIBLIA

Inafundisha Kuhusu...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,

Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,

I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt.

25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa 1)

ameonyeshwa maono ya “nyota saba....na ya vile vinara saba” (Ufunuo 1:20). Akaambiwa kwamba nyota hizo zilikuwa malaika wa yale makanisa saba. Basi nyota hizo zinawakilisha wahudumu wa Injili ambao wanaitwa “malaika” au wenye kubeba ujumbe. Ndiposa nyota kumi na mbili za taji la mwanamke yule ni huduma ambayo ilibeba ujumbe wa injili na kupeleka kwenye ulimwengu uliopotea. Watumishi wakuu zaidi kwenye huduma hiyo ya kwanza ilikuwa ni mitume wale kumi na wawili ambao walifanya bidii tangu mwanzo kushiriki mwangaza wa ukweli. “Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni” (Waefeso 2:19-20).

“Makanisa” mengi na dini nyingi zimefanya uzinzi wa kiroho na kufanya ukahaba kwa mambo ya dunia. Makanisa yanasujudu miungu ya kizazi hiki na kukubaliana na falsafa na matendo ambayo ndani mwake mmejaa dhambi. Imani za kibinadamu zinachukua mahali pa Neno la Mungu lililoandikwa. Makanisa haya hayadumishi uaminifu kwa bwana-arusi ambaye ni Yesu Kristo. Kanisa la kweli la Mungu limechumbiwa kwa mume mmoja na litatolewa kwa Kristo kama bikira (2 Wakorintho 11:2). Ni shauku lake Bwana “apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa” (Waefeso 5:27). Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya bi-arusi huyu mrembo wa Kristo ambaye anajidumisha akiwa safi na bila mawaa ya ulimwengu na mwenye utukufu wa mwangaza wa Neno la Mungu.

—mws

UKWELI WA INJILI

Gazeti la ‘Ukweli wa Injili’ huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

UAGIZAJI

Ukweli wa Injili ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuoongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

WASILIANA NASI

Gazeti a Ukweli wa injili linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

Ukweli wa Injili, PO Box 2042., Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

Tahariri



Kwa ajili ya Sayuni sitanyamaza, na kwa ajili ya Yerusalemu sitatulia, hata haki yake itakapotokea kama mwangaza, na wokovu wake kama taa iwakayo.
—Isaya 62:1

Somo la muhula huu wa robo ya mwaka ni kuhusu “Kanisa.” Shauku kubwa la moyo wangu ni kwamba kila mtu aliye na ukweli atapata maono ya urembo wa kanisa la kweli la Mungu. Nyingi za taasisi za kidini na mashirika ya Wakristo yamedunisha ukweli hivi kwamba Wakristo wanapata ujumbe kwamba hawana haja ya “kuchukua msalaba wao kila siku” kulingana na jinsi Bwana alivyofundisha. Njia ya kumtumikia Bwana ni nyonge na ni ya utakatifu lakini ni njia nzuri. Ni njia ambayo inamwongoza mtu kupata nguvu na ushindi. Tukiruhusu ukweli kuhusu kanisa la Mungu kuwa maishani mwetu na katika ushirika wetu ni jambo litakalomletea Mkristo uhuru na uwazi wa kuabudu “kwa roho na kweli.”

Watu wengi hawatakubali kwamba wao ni sehemu ya kanisa la mwanadamu, lakini mtu akijifunza maandiko hatakosha kutambua kwamba makanisa mengi sio sehemu ya kanisa moja la kweli la Mungu. Mungu aliweka wazi mipangilie ya Kanisa lake. Sio kazi yetu kufanya mpangilie huo kuwa wa kisasa. Ni kazi yetu na mwito wetu kujipima kwa Neno la Mungu. Kanisa la Mungu lina urembo na utukufu. Kama Mlima Sayuni kanisa hilo huinuka juu ya mawingu yanayoleta hali ya kuchanganyikiwa ambayo imetandaa katika ulimwengu wetu wa kidini.

Ni baraka kubwa mtu kuwa huru kutokana na dhambi na kuwa huru kutokana na mafundisho na tamaduni za kibinadamu. Haitoshi mtu kuwa na ufahamu wa ukweli katika akili zake tu. Ukweli huo unahitaji kutumiwa kwa mambo ya kila siku ili mwili wa kweli wa Kristo uweze kujidumisha bila kuingiliwa na mawaa ya kilimwengu. Makanisa mengi hujiita “Kanisa la Mungu,” lakini jina peke yake halitoshi. Je, Roho wa Mungu ndiye anayeongoza mambo kanisani humo ama ni mwanadamu anaongoza? Je, Biblia ndio mwongozo mkuu kwa mambo ya imani ama tu ni vile ambavyo mhudumu wa kanisa anavyosema? Je, kuna mpangilie wa mamlaka pale kanisani ama kweli Kristo ndiye kichwa cha kanisa hilo? Bwana atusaidie ili tuweze kufa kwa ajili ya nafsi zetu wenyewe ili kanisa liweze kuwa “Mji ulio kwenye Mlima” ambao hauwezi kufichika.

Sisi hatuhitaji kuwa waaminifu kwa historia iliyopita ama kwa maisha ya kitamaduni peke yake. Watu wengi hata katika “Kanisa la Mungu” wako huko kanisani kwa sababu walilelewa hivyo. Lakini mtu kuwa mshirika katika kanisa la Mungu ni jambo linalofanyika wakati ambapo moyo wa mtu unabadilishwa kwa nguvu za kiungu. Uaminifu wetu unahitaji kuwa kwa Mungu Mwenyewe na kwa Neno lake la kiungu ambalo linatuwezesha kutembea katika utakatifu katika maisha ya kila siku.

Kama nitakavyoongozwa na Bwana mimi nitaweza kushughulikia mambo kadhaa ya *maisha* ya kila siku yanayotokana na umoja na ushirika wa kanisa kwenye matoleo ya baadaye ya jalida hili.

Ewe rafiki yangu mimi ninakuomba kuwa mtu mwaminifu, kwa maana punde si punde Bwana anarudi.

Michael W. Smith

Oktoba 2013



Tutembelee kwa

www.thegospeltruth.org

ili uagize na kusoma

jarida letu.

MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

SOMO: KANISA LA MUNGU

Kuna

MOJA

Mwili

Roho

Tumaini

Bwana

IMANI

Ubatizo

MUNGU

Baba

Mafundisho

JINA

Waefeso 4:4-5

2 Timotheo 3:16-17

Waefeso 3:14-15

Somo la Biblia:...*Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.* –
Matendo 2:47

Muhstasari: Kanisa ni taasisi ya kiungu ambalo lilianzishwa na Kristo, linaongozwa na Roho, na Neno la Mungu ndilo mwongozo wake kwa mambo ya imani. Washirika wa Kanisa la Kibiblia—Kanisa la Mungu, ni waumini wote ambao wameokolewa kutokana na dhambi.

Maana: Neno “kanisa” linatokana na neno la Kiyunani “eklesia” ambalo lina maana ya “kusanyiko” ama “walioitwa kutoka.”

I. Mwanzilishi na Mjenzi

- A. Mathayo 16:15-18 Mjenzi ni Kristo.
- B. Waebrania 8:1-2 Haikujengwa na mwanadamu.

II. Msingi na Mlango—Yesu

- A. 1 Wakorintho 3:9-11 Msingi.
- B. Waefeso 2:20 Jiwe kuu.
- C. Yohana 10:7-9 Lango la pekee la kupata wokovu.

III. Washirika Wake

- A. Matendo 2:46-47 Wote walio-okoka.
- B. 1 Wakorintho 1:2 Watakatifu.
- C. 1 Wakorintho 12:18 Mungu humweka kila mshirika mahali pake.
- D. 1 Yohana 5:18 Washirika wake hawatendi dhambi.

IV. Daftari ya Washirika

- A. Luka 10:20 Majina yameandikwa mbinguni.
- B. Wafilipi 4:3 Kitabu cha Uzima (Ufunuo 20:12).

V. Kichwa—Kristo

- A. Waefeso 1:22 Kichwa juu ya vitu vyote.
- B. Waefeso :23-24 Kichwa cha kanisa (Waefeso 4:15-16).
- C. Wakolosai 1:17-19 Kichwa cha mwili.
- D. Isaya 33:20-22 Hakimu na mwenye kutoa sheria.

VI. Kanuni au Mwongozo wa Imani

- A. 2 Timotheo 3:16-17 Maandiko yote.
- B. 2 Petro 1:21 Yamevuviwa.

VII. Mpangilie

- A. 1 Wakorintho 12:18, 27-28 Mungu huweka kila mshirika mahali pake.
- B. Waefeso 4:10-13 Mungu hutoa karama.
- C. 2 Wakorintho 3:5-6 Mungu ndiye huwatosheleza wahudumu wa Kanisa.

VIII. Jina la Kibiblia

- A. Waefeso 3:14-15 Limepewa jina la Baba.
- B. Waefeso 4:10-13 Lisha kanisa la Mungu.
- C. 2 Wakorintho 1:1 Kanisa la Mungu la Korintho (1 Wathesalonike 2:14).

IX. Kanisa Moja

- A. Warumi 12:4-5 Mwili moja ndani ya Kristo.
- B. Waefeso 4:4-6 Imani moja.
- C. 1 Wakorintho 12:12-14, 20 Viungo vingi lakini mwili mmoja.

X. Maelezo kuhusu Kanisa

- A. Waefeso 1:22-23 Mwili wa Kristo.
- B. 2 Wakorintho 11:2 Bi-arusi wa Kristo.
- C. Waebrania 12:22-23 Mji wa Mungu – Mlima Sayuni.
- D. 1 Timotheo 3:15 Nguzo na Msingi wa Ukweli.

KANISA LA MUNGU

Nakala ya kuandamana na Mafunzo ya Biblia

KANISA NI TAASISI LA KIUNGU LA MUNGU

Kweli za kawaida kuhusiana na kanisa zinaangazia mapenzi na kusudi za Mungu katika maisha haya na pia kudhihirisha uongo wa taasisi za kidini katika jamii zetu. Ulimwengu umejaa dini na makanisa yenye viwango mbali mbali na imani tofauti. Hata ingawa watu wengi katika siku zetu huendeleza dhana kwamba “kila mtu ana haki ya kuhudhuria kanisa lolote alilochagua yeye mwenyewe” Biblia hufundisha kwamba kuna njia moja tu nyembamba ambayo huongoza mtu kwenye uzima (Mathayo 7:13-14).

MAANA YA ‘KANISA’

Kanisa linatajwa mara ya kwanza katika Biblia kwenye Mathayo 16:18, “Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.” Neno *kanisa* linatokana na neno la Kiyunani *ekklesia* ambalo lina maana ya “kusanyiko” ama “walioitwa kutoka.” Maandiko yanatumia tena neno *kanisa* katika Matendo 2:47, “Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.” Kanisa silo jengo au mahali pa ibada, kanisa ni watu ambao wameokolewa kutokana na dhambi zao. Watu wa Mungu wameitwa ili “watoke” dhambini, watoke duniani, watoke kwa dini, n.k. Wao wana ushirika na Mungu na umoja wa Roho, huku wakiishi kwa imani katika Neno la Mungu.

WASHIRIKA WA KANISA LA KWELI LA MUNGU


Mtu kuwa mshirika wa kanisa hakutokani na yeye kuhudhuria ibada, ama kwa kuandikwa kwenye kitabu cha washirika wa kanisa, ama kwa yeye kupata cheti cha ubatizo. Mungu ndiye huweka washirika kwenye mwili (1 Wakorintho 12:18). Tunaingia kanisani mwa Mungu tunapozaliwa tena na kuokolewa kutoka dhambini kwa damu yake Yesu Kristo ambayo hutupatanisha na Mungu.

Kila mtu katika kanisa la Mungu anaishi huku akiwa huru kutokana na dhambi.

YESU NDIYE MLANGO WA PEKEE

Yesu ndiye mlango wa pekee ambao tunaweza pitia ili kuingia kanisani mwake. Yeye peke yake ndiye mwenye uwezo wa kusamehe dhambi, “. . . mtu akiingia kwa mimi, ataokoka . . .” (Yohana 10:9). Hakuna kikundi cha watu, kuhani, askofu, au mhudumu yeyote wa Injili mwenye

uwezo huo. Basi hakuna mtu ambaye anaweza kutuingiza kanisani na hakuna mtu anaweza kututoa hapo. Kitabu chenye washirika wa kanisa kimewekwa mbinguni (Luka 10:20) na majina yake yamewekwa katika kitabu cha uzima (Wafilipi 4:3). Na kwa sababu Mungu anajua kila mtu na kila moyo nakala ya washirika wa kanisa liko sawa, na hakuna jina lililoachwa nje.



KANISA LA MUNGU

Kanisa silo jengo . . . washirika wake ni watu wote ambao wameokolewa kutokana na dhambi.

YESU NDIYE MWANZILISHI

Kanisa la Mungu lilianzilishwa na kujengwa na Yesu Kristo Mwenyewe, “. . . nitalijenga kanisa langu” (1 Wakorintho 13:11). Kikundi chochote cha kidini ambacho kinaashiria kwamba mwanadamu fulani ndiye mwanzilishi hakifuati ukweli. Mwandishi mmoja anayeitwa Circa aliandika katika mwaka wa 30 (Baada ya Kristo) na kusema

kwamba Yesu ndiye alianzisha kanisa lake humu duniani, si mwanadamu (Waebrania 8:1-2). Yeye alikufa, akafufuka, akapaa kwenda Mbinguni na kumtuma Roho Mtakatifu ili awape nguvu waumini za kuishi maisha matakatifu.

MSINGI WAKE NI KRISTO

Yesu ndiye msingi wa taasisi hii ya kiungu: “Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo” (1 Wakorintho 3:11). Neno la Mungu lililovuviwa ndilo kanuni au mwongozo wa pekee wa imani katika kanisa la Mungu

(Inaendelea kutoka ukurasa 6)

(Endelea kutoka ukurasa 5)

(2 Timotheo 3:16-17). Maandiko ndiyo hupewa kipa umbele na mamlaka yake ni ya juu zaidi ya kila tamaduni, mazoea, au tamko la imani ya kibinadamu. Katika kanisa la Mungu hamna kundi la askofu la kuwachagua viongozi au wahudumu wa Injili ambao ndio huamua mpangilie wa kanisa. Mungu tayari ashatupatia Neno lake na Roho wake kuwa mwongozo wa maisha yetu.

KRISTO HANA MBADALA

Yesu ndiye “. . . kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; . . . ili kwamba awe mtangulizi katika yote” (Wakolosai 1:18). Hakuna mbadala wake Kristo mbinguni na duniani. Yeye ndiye kichwa cha kila kitu. “Kwa maana Bwana ndiye mwamuzi

wetu; Bwana ndiye mfanya sheria wetu; Bwana ndiye mfalme wetu; ndiye atakayetuokoa” (Isaya 33:22). Katika kanisa la Mungu hamna nafasi ama haja ya uchaguzi wa askofu au msimamizi kwa maana Kristo ndiye askofu wa nafsi zetu.

VIONGOZI HUCHAGULIWA NA MUNGU

Katika kanisa la Mungu ndiye huweka washirika mwilini kwa jinsi apendavyo (1 Wakorintho 12:18). Yeye ndiye hupatia kanisa karama (Waefeso 4:10-13) na Roho hupanga na kuongoza kanisa kulingana na mapenzi Yake. Mara nyingi mwanadamu hujaribu kuchukua wajibu huo wa kuongoza na kuchagua. Lakini katika mwili wa Kristo washirika humtegemea Roho kuwaongoza kwa njia watakayofuata. Upako wa Roho na uongozi hauji kwa njia ya elimu, au kwa kuhudhuria seminari, au kwa kuwa na uhusiano na mtu fulani aliye uongozini bali kwa mtu kujitoka wakfu kwa wito wake Mungu.

KANISA LILIPEWA JINA LAKE NA MUNGU MWENYEWU

Kuna majina mengi na maelezo ya vyeo vya kanisa na taasisi za kidini. Lakini tayari Mungu amewapatia watu wake jina. “Kwa hiyo nampigia Baba magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa” (Waefeso 3:14-15). Ni aibu kwa familia ya kiroho kuitwa kwa jina lingine isipokuwa

lile la baba yake. Neno la Mungu liliwafunza wahudumu wa Injili wapate “kulilisha kanisa lake Mungu” (Matendo 20:28). Jina la kweli na la kibiblia la kanisa ni “Kanisa la Mungu.” Katika Maandiko waumini wa mahali pamoja waliitwa Kanisa la Mungu (2 Wakorintho 1:1). Ingawa jina peke yake halimwoko

mtu hilo ndilo jina ambalo limepewa kanisa la Mungu. **KANISA NI MOJA** Ingawa kuna makanisa mengi sana na dini



Kanisa la Mungu halipangwi na kamati za watu au kwa uchaguzi bali linatawaliwa na Roho Mtaktifu.

nyingi Mungu ana kanisa moja tu – Kanisa la Mungu. Kanisa hilo hujulikana kama “mwili wa Kristo” (Efeso 1:22-23). “Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo” (1 Wakorintho 12:12). Maandiko pia yanasema kwamba Kanisa ni bi-arusi (2 Wakorintho 11:2). Mungu hana mabibi wengi. Yeye ana bi-arusi mmoja ambaye ni kanisa.

Tunamuomba kila msomi atambue tofauti kati ya kanisa la kweli la Mungu na makanisa ya wanadamu. Kanisa la Mungu ni huo mji ambo umewekwa juu ya kilima na ambao hauwezi kufichika (Mathayo 5:14). Kanisa hili limepaa juu ya hali zote za kuchanganyikiwa kwa wanadamu kuhusiana na maswala ya kidini na mafundisho ya kidini. Kanisa la Mungu ni safi, takatifu, lisilo na doa, na la kweli. Kristo ndiye mwanzilishi, kiongozi, mwenye kutoa sheria, na Mwokozi wake.

—mws

SWALI na JIBU

Swali: Kanisa ambalo mimi huhudhuria halifunzi ukweli wote unaopatikana kwenye Biblia. Je, nifanye nini kuhusiana na jambo hilo.

Jibu: Hili ni swali lenye umuhimu mkubwa na nzito ambalo linastahili jibu lililowaziwa vizuri kwa maana watu wengi hujipata kwenye hali kama hii. Ni muhimu kutambua kwamba Kanisa la Mungu ni kanisa la kiungu. Kila mtu ambaye ameokolewa kutoka dhambini kupitia kwa Yesu Kristo huwa ni sehemu ya kanisa hilo la kweli (Matendo 2:47).

Kuhudhuria ibada katika kusanyiko la dhehebu yoyote ile na lililo na jina lolote lile hakumleti mtu katika taasisi ya kiungu inayoitwa kanisa. Mtu yeyote ulimwenguni ambaye hutubu dhambi zake huweza kuingia kanisani. Yeye anaweza kujitambulisha kama mshirika wa “kikundi” fulani lakini kundi lenyewe silo ambalo Mungu hutambua. Mtu mwenyewe hufanyika kuwa mshirika wa Kanisa la Mungu, iwe anatambua hivyo ama hatambui, kwa maana Mungu hutambua hali ya moyo na maisha ya mwanadamu.

Taasisi yoyote au “kanisa” ambalo halifunzi ukweli wote linaweza kuziletea nafsi za watu hasara kubwa. Ni kweli kwamba watu wanaweza kuokoka kwa njia ya mahubiri kanisani humo kama kutakuwa na toba ya kweli. Lakini shida ya kuendelea kushiriki kwenye kanisa hilo huwa kwamba inakuwa ngumu

kuendelea kuwa “mwokovu” kwa maana hadaa za kiroho ni moja ya matokeo ya kudumu kutokana na mafundisho ya uongo. Hamna shaka kwamba “kanisa” ambalo linafunza uongo na ambalo limepotoka kwa mambo ya ukweli wa Neno la Mungu ni kanisa ambalo limeanguka machoni pake Bwana. Maandiko huita makanisa kama hayo kuwa ni Babiloni, ama yaliyochanganyikiwa. Katika kitabu cha Ufunuo makanisa hayo yamepewa mfano wa “kahaba” na hayamruhusu Roho wa Mungu kuwaongoza. Imani zao kuhusiana na dini huchukuliwa kuwa muhimu zaidi kuliko Biblia yenyewe. Kamati zao za kanisa nazo



JE, NINASTAHILI KUSHIRIKI KATIKA KANISA LA UONGO?

huchukua mahala pa Roho Mtaktifu, n.k. Utaratibu huo ni mpotovu naye Mungu haukubuli. Ndiposa Maandiko yanasema, “...Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake...” (Ufunuo 18:4).

Shetani ameleta madhara makubwa kwa Ukristo wa kweli kupitia kwa makanisa yanayojiita ya Kikristo hata kuliko alivyofanya kupitia kwa makafiri na kwa mateso ya moja kwa moja ambayo ameiletea kanisa. Makanisa yanayofundisha sehemu sehemu za

ukweli na hayafundishi ukweli wote ni hatari zaidi kwa watu wanaotafuta ukweli kuliko dini ambazo zinafundisha kinyume na Biblia. Ukweli ambao sio kamili huacha pengo ambazo adui hufanya kazi maishani mwa Wakristo. Mapenzi yake Bwana ni kwamba tujitenge kutokana na manabii wa uwongo na kutokana na taasisi za kibinadamu na tuwe katika ushirika na washirika wa kweli wa mwili Kristo— maanake Kanisa la Mungu.

Ingawa mifumo na misingi ya makanisa mengi hayafai kwa sababu hayafundishi ukweli wote ni muhimu kutambua kwamba kuna watu wengi wasio na makosa ambao wako na wanadumu kwenye mifumo hiyo. Mradi watu hao wataishi maisha matakatifu mbele zake Mungu wao wataenda mbinguni watakapoaga dunia. Lakini mtu akiendelea kudumu katika mahubiri ambayo si ya ukweli wote atapata madhara kwa jinsi ambavyo ataendelea kudumu humo. Mwisho wao watajipata kwenye njia panda na itawabidi kujjuliza – “Je, mimi niendeleo kudumu chini ya mahubiri haya yasiyo ya kweli na kuyakubali tu, ama niwe wazi mbele zake Bwana na nijitenge kutokana na mambo yaliyo mapotovu?”

Jinsi swali hivyo litakavyoshughulikiwa litaleta tofauti ya hatma ya maisha ya milele ya mtu. Watu wanahitaji

kusimama wima kwa unyenyekevu dhidi ya uongo na kuwa kwenye ushirika na umoja wa imani na wa Roho.

Ni ombi letu kwamba Bwana atapatia neema na hekima nyingi yeyote yule aliye kwenye dini za uongo na awape ujasiri wa kusimama wima kwa kile ambacho ni cha haki na cha kweli. Amina.

—mws



JE, WAJUA?

Ukweli kuhusu Mtume Petro . . .

- Jina lake lilikuwa Simoni Bar-yona, Yesu naye akampatia jina lingine Kefa (Petro), maanake jiwe.
- Alizaliwa Bethsaida, karibu na Bahari ya Galilaya na kikazi alikuwa mvuvi wa samaki.
- Petro alikuwa mmoja wa wanafunzi wale kumi na wawili na alikuwa ameoa.
- Ndugu yake alitwa Andrea na alikuwa mfuasi wa Yohana Mbatizaji, halafu akawa mtume wa kwanza wa Yesu.
- Alikufa hapo mwaka wa 64 (Baada ya Kristo) huko Roma katika utawala wa Kaisari Nero. Yeye alisulubiwa kichwa chini miguu juu kwa maana hakuona kwamba anastahili kufa kwa njia moja na Bwana wake Yesu.



**Neno
Linalofaa kwa
Msimu Huu**

Yehova-Nisi—Bwana ni Bendera Yangu

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA
Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Kutoka 17:15 Musa akajenga madhabahu, akaiita jina lake Yehova-nisi.

Wakati Musa angeinua mikono juu wana wa Israeli wangeshinda Waamaleki vitani. Ndiposa Haruni na Huri wakasimama kando kando yake Musa ili wamshike mikono kuinanyua hewani wakati Musa alipochoka. Basi Mungu akawapatia ushindi dhidi ya adui. Kwa kumbukumbu la jambo hilo Musa akajenga madhabahu na kuyaita Yehova-nisi, maanake “Bwana ni bendera yangu.”

Kuna sababu nyingi zinazofanya askari kuinua bendera ya kuwaongoza vitani. Bendera hiyo ilitumika kutambua watu, kupeana mwongozo vitani, kuwapatia askari motisha, na kama ishara ya ushindi. Wana wa Israeli hawakupigana kibinafsi, wao walikuwa wakipigana kama mwili wenye umoja chini ya uongozi wa Bwana Mungu. Yehova alikuwa ndiye bendera yao. Waisraeli walishinda kwa jina lake.



Wakati mwingi moshi na kelele za vita huleta ukungu machoni pa watu na kuwakosesha uwezo wa kuona maono na mwelekeo wa vita. Jambo hilo pia ni kweli katika vita za kiroho ambazo tunakumbana nazo maishani mwetu. Ikiwa tutatazama sana mazingara yaliyotuzunguka tunaweza kufa moyo na kukatishwa tamaa. Tunahitaji kutafuta na kusimama wima tukiwa na bendera yetu. Kristo ndiye muhuri wetu (Isaya 11:10) na tunafanya kazi katika mapenzi, bidii, na kujitoa mhanga kwake. Sisi tunaweza kutambulika tu kwa jina hilo la Yehova-nisi, na ni ndani yake tu ndipo tunaweza kupata kusudi, nguvu mpya, na hata ushindi.

—mws